**BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA**

**MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU KIDATO VI**

**KISWAHILI 2**

**121/2** **(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)**

**MUDA: SAA 3** **Jumanne Machi 5, 2024 Asubuhi**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **nane (8).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka sehemu A na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B. Swali la **saba (7)** ni la lazima.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60).**
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
5. Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba** yako ya **Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Uwiano wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi simulizi hupelekea katika kujenga kazi bora na yenye tija kwa jamii. Kwa kutumia hoja tano (5) eleza uhusiano huo kwa mifano.

2. Mzee Hadithi ametokana na kizazi cha ukoo wa Fasihi simulizi na kizazi cha Fasihi simulizi kimetokana na kizazi cha Fasihi. Fafanua watoto wa Mzee Hadithi wanaoendeleza kizazi cha Fasihi.

3. Mtunzi wa kazi ya fasihi huhitaji uhuru ili aweze kutunga kazi iliyo bora kwa maslahi mapana ya jamii. Kwa kutumia mifano eleza vikwazo vitano (5) vinavyoingilia uhuru wa mtunzi wa kazi ya fasihi na kumfanya ashindwe kutunga kazi ya fasihi iliyokuwa bora kwa jamii yake.

4. Soma matini ifuatayo, kisha eleza mbinu tano (5) za kifani zilizotumika kuunda matini hii kwa kutoa mifano kwa kila mbinu.

| | |
|---|---|
| CHUKU : | (anaanza kulia). |
| SIKITU : | Eeh! Ukweli unauma sasa …….. |
| MAMA CHUKU: | Aaa, Baba Juma, usimfikirie mtoto mambo mabaya. |
| SIKITU : | Hapana. Huyu mtoto amekwishaanza kuharibika, mara nyingi nimeandikiwa barua na baba yake mdogo kusema Chuku hatulii, na wewe hukuamini ukasema wanaanza kumsingizia mtoto wako, mpaka tukagombana na aliyekuwa anatusomea barua zetu. (Mara hodi inasikika). Ehee! Sasa utaniona, nitamnyoosha barabara. (Anachukua fimbo yake iliyokuwa imeegemea ukutani na anakwenda karibu na mlango na anainua fimbo kungojea ishuke mara tu apigaye hodi atakapoingia.) |
| MAMA CHUKU: | Hapana baba Chuku! (Anamshika lakini anamsukuma) sio vizuri. |
| SIKITU : | Sogea huko! (Mgeni anaingia na fimbo ya Mzee inashuka na kutua begani mwake). Wewe ndiye …… |
| CHIPEPE : | (Anaanguka kwa uchungu na barua alizoshika zinatapakaa chini) Ochchch! Mzee vipi? Nimekukosea nini? Ahaa. (Akainuka na kushika bega lake. Ndipo Saidi anaona kosa lake. Chuku baada ya kuona barua anatoka). |

| | |
|---|---|
| SIKITU : | Ooh! Pole sana mwanangu, sikujua kuwa ni wewe. Tulikuwa tunamtegemea mpumbavu mmoja, lakini bahati yake. Pole sana mwanangu! (anasaidia kuokota barua). |
| CHIPEPE : | Loo! Pameuma. Pole tu haisaidii kitu. Mzee siku nyingine uwe na uhakika au la tutaogopa kukuletea barua zako. Unaonesha kuwa ni mkali sana! Sana! Sana! |
| SIKITU : | (Huku akicheka): Ehee … Ehee ….. wazee wakati mwingine huwa tuna hasira. Kuna barua yetu? Kutoka Dali salaam? |

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka katika sehemu hii. Swali la **saba (7)** ni la lazima.

ORODHA YA VITABU

**USHAIRI**

| | | |
|---|---|---|
| Kimbunga | - | Haji Gora |
| Mapenzi Bora | - | Shabaan Robert |
| Fungate ya Uhuru | - | M.S Khatibu |
| Chungu Tamu | - | T.A. Mvungi |

**RIWAYA**

| | | |
|---|---|---|
| Kufikirika | - | Shabaan Robert |
| Mfadhili | - | Hussein Tuwa |
| Vuta N'kuvute | - | Shafi A. Shafi |
| Usiku Utakapokwisha | - | Mbunda Msokile |

**TAMTHILIYA**

| | | |
|---|---|---|
| Kwenye Ukingo wa Thim | - | E. Hussein |
| Kivuli Kinaishi | - | S. Mohamed |
| Nguzo Mama | - | P. Muhando |
| Morani | - | E. Mbogo |

5. Watunzi wazuri wa kazi za kifasihi katika dunia ya leo ni kichocheo cha mabadiliko chanya kutoka katika jamii zao. Kwa kutoa hoja nne (4) kwa kila diwani ulizosoma, fafanua namna wanavyochochea katika kuleta mabadiliko chanya katika jamii za Kiafrika.

6. “Nguo hununuliwa dukani na mapenzi hutoka moyoni na sio kulazimishwa na fulani.” Jadili kauli hii kwa kutoa hoja nne (4) kwa kila riwaya kati ya riwaya mbili ulizosoma.

7. Watunzi wa kazi za fasihi hupendelea kutumia zaidi mitindo katika kuumba kazi zao ili kufikisha ujumbe waliokusudia kwa jamii husika. Kwa kutoa hoja nne (4) kwa kila tamthiliya, onesha namna watunzi walivyotumia mitindo kufikisha ujumbe kwa jamii.

8. “Wasanii ni mafundi wazuri sana wa kusawiri jazanda ili kufikisha ujumbe kwa jamii.” Tumia diwani mbili ulizozisoma kwa kutoa hoja nne (4) kwa kila diwani kujadili kauli hii.

*Wabillah Tawfiiq*